# Kalenda ya kilimo bora cha

# Mpunga

## Halmashauri ya wilaya ya Iringa – Idodi



## Vijiji vya Idodi, Nyamahana, Malinzanga, Tungamalenga na Mapogolo

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE
IITA Transforming African Agriculture CGIAR
ACDI VOCA Expanding Opportunities Worldwide
TARI
FEED THE FUTURE The U.S. Government's Global Hunger & Food Security Initiative

# Mwezi Septemba

## Maandalizi ya msimu mpya wa kilimo

### Matukio

- Endelea kuuza sehemu ya mazao kwa bei ya soko
- Andaa mpango wa msimu mpya wa Kilimo
- Hakikisha ukubwa wa Shamba tarajiwa unajulikana




Kupanga kwa msimu mpya wa kilimo

# Mwezi Oktoba

## Kununua pembejeo na maandalizi ya shamba

### Matukio

- Endelea kuuza sehemu ya mazao kwa bei ya soko
- Nunua pembejeo kwa kuwasiliana na mshauri wa kilimo kijijini kwako-VBAA, au kwa ushauri toka afisa ugani
- Tunza pembejeo sehemu salama.




Kununua pembejeo

# Mwezi Novemba

## Kuandaa shamba

### Matukio

- Endelea kuuza sehemu ya mazao kwa bei ya soko
- Safisha shamba kwa ajili ya msimu mpya wa kilimo
- Pembejeo zilizonunuliwa zitunzwe sehemu salama (Isiyo na unyevu, iwe mbali na watoto, isiyo na jua kali na isiyofikiwa na panya)



Kusafisha shamba

# Mwezi Desemba

## Maandalizi ya majaruba na vitalu

### Matukio

- Andaa matuta ya majaruba kwa upana wa kati ya sm 120-160 kwa chini, urefu kwenda juu (kina) kati ya sm 40-50, na upana wa juu kati ya sm 30-50 (sm = sentimeta)
- Hakikisha shamba lina majaruba na mifereji ya kuingiza na kutoa maji
- Katua, chabanga/vuruga na sawazisha shamba lako vizuri
- Sia mbegu bora kwenye vitalu (usitumie mpunga uliovuna shambani kama mbegu)
- Tunza vitalu kwa kumwagilia maji, kupalilia na kudhibiti visumbufu
- Endelea kuuza sehemu ya mazao kwa bei ya soko



Maandalizi ya majaruba

Picha A: Kuandaa vitalu



# Mwezi Januari hadi Januari

## Kupandikiza miche shambani

### Matukio

- Hakikisha jaruba lina kina cha maji kisichozidi sm 3
- Pandikiza miche shambani ikiwa na siku 14-21, kwa nafasi ya sm 20 mche hadi mche na mstari hadi mstari
- Pandikiza miche kuanzia mmoja hadi mitatu kwa shina
- Weka mbolea ya kupandia kwa kiwango na wakati sahihi kulingana na ushauri wa afisa ugani na VBAA (Wakati wa maandalizi ya mwisho ya shamba au ndani ya siku tano baada ya kupandikiza)
- Rudishia miche kwenye nafasi ambazo miche imekufa ndani ya siku 10 baada ya kupandikiza
- Endelea kuuza sehemu ya mazao kwa bei ya soko



Kupandikiza miche shambani

# Mwezi Februari

## Kuweka mbolea ya kukuzia

### Matukio

- Hakikisha shamba halina magugu kabla ya kuweka mbolea
- Hakikisha shamba lina kina cha maji kisichozidi sm 5
- Weka mbolea ya kukuzia ndani ya siku 14 baada ya kupandikiza, kutokana na ushauri wa VBAA au afisa ugani.




Uwekaji wa mbolea ya kukuzia

## Kudhibiti maji na visumbufu

### Matukio

- Ondoa magugu shambani mara tu yanapoonekana kwa kutumia mbinu husishi kama vile kupalilia kwa mshine, vipalizi vya mkono, viuatilifu na kung'olea
- Dhibiti wadudu waharibifu na magonjwa mara tu yanapoonekana kwa kutumia mbinu husishi, kama vile viuatilifu au mbinu za asili
- Endapo utatumia viuatilifu weka kiwango sahihi kulingana na ushauri wa VBAA au afisa ugani
- Usiache vifungashio vya viuatilifu shambani; peleka sehemu maalum iliyotengwa kwa ajili ya kukusanyia vifungashio hivyo
- Hakikisha kina cha maji hakizidi sm 15 wakati wote wa ukuaji




Picha A: Kudhibiti magugu kwa kutumia kipalizi cha mkono




Picha B: Kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa kwa viuatilifu

## Kuweka mbolea ya kuzalishia

### Matukio

- Weka mbolea ya kuzalishia kwa viwango sahihi kulingana na ushauri wa VBAA au afisa ugani
- Weka mbolea mpunga unapoanza kurefuka pingili (au kubeba mimba)
- Endelea kudhibiti visumbufu kadri vinapojitokeza
- Usiache vifungashio vya viuatilifu shambani; peleka sehemu maalum iliyotengwa kwa ajili ya kukusanyia vifungashio hivyo



Kuweka mbolea ya kuzalishia

## Kudhibiti ndege na wanyama waharibifu na kuvuna

### 1. Kudhibiti ndege na wanyama waharibifu

**Matukio**

- Tumia njia za kiasili kutisha na kufukuza ndege na wanyama waharibifu
- Dhibiti panya kwa kutumia sumu na njia za asili
- Usiache vifungashio vya viuatilifu shambani; peleka sehemu maalum iliyotengwa kwa ajili ya kukusanyia vifungashio hivyo



Mbinu za asili za kutisha na kufukuza ndege

## 2. Maandalizi ya kuvuna

### Matukio

- Nunua vifungashio vya kuhifadhia mavuno mapema (magunia, maroba)
- Jenga au karabati ghala la kuhifadhia mazao
- Andaa mashine za kuvunia, za kupura mpunga na maturubai ya kuanikia mpunga






Maandalizi ya maghala ya mavuno na vifungashio

# Mwezi Aprili hadi Mei...


## 3. Kuvuna na kupura

### Matukio

- Vuna kwa wakati suke likiwa limekomaa kwa asilimia kati ya 80 na 85 au tumia kipima unyevu kutambua unyevu wa punje (asilimia kati ya 20 na 25)
- Kata mashina ya mpunga kwa kutumia fyekeo au kwa mashine (kupunguza upotevu wa mpunga)
- Endapo umetumia fyekeo, pura mpunga kwa kutumia mashine ili kuongeza ubora wa mpunga na kuokoa muda
- Usiache mpunga uliovunwa shambani na magunia yafungwe vizuri tayari kwa kusafirishwa
- Tenganisha aina za mpunga katika magunia tofauti ya kilo mia moja
- Kausha mpunga hadi unyevu wa punje ufikie asilimia 14




**Picha A: Uvunaji mpunga kwa fyekeo**




**Picha B: Uvunaji mpunga kwa mashine (Kombaini)**




**Picha C: Kupura mpunga kwa mashine**




**Picha D: Usafirishaji mavuno toka shambani**

# Mwezi Juni hadi Agosti

## Kuhifadhi ghalani na kuuza

### Matukio

- Kusanyeni na kuhifadhi mpunga kwa pamoja kwenye ghala la kikundi au ushirika
- Tenganisha magunia kulingana na aina ya mpunga ili kulinda UBORA
- Hakikisha magunia ya mpunga yamepangwa kwa utaratibu mzuri juu ya mbao
- Fanyeni maamuzi ya pamoja ya kuuza mavuno ili kupata bei nzuri na kwa FAIDA



Kuhifadhi ghalani kwa pamoja



Kupanga bei kwa pamoja



Kuuza kwa pamoja kwa faida zaidi

Mradi huu unaohusisha Afrika RISING, NAFAKA, na TUBORESHE CHAKULA wadau na sekta mbalimbali kwa nia ya kuongeza kasi ya utekelezaji na kukuza teknolojia mbalimbali za kuwasaidia wakulima wa Tanzania walioko katika maeneo ya ukame na yale yenye mvua kidogo. Mradi huu ni wamiaka 3 na unawezeshwa na shirika la misaada la Marekani ofisi ya Tanzania (USAID) ikiwa ni sehemu ya juhudi za serikali ya Marekani katika jitihada zake za kuboresha usalama wa chakula.

Kupitia njia shirikishi za kilimo tekinolojia bora zinazofaa huchaguliwa na kufanyiwa utafiti na tathimini na watafiti ili kuweza kufikia maeneo mengi zaidi. Hili linafanyika kwa ushirikiano uliopo kati ya programu za 'Feed the Future'; NAFAKA, TUBORESHE CHAKULA na wadau wengine kwa kutoa fursa kuhuwisha katika miradi na maeneo mengine ambapo mradi wa Africa RISING haujafika.

Mradi huu unatekelezwa na IITA kwa kushirikiana na miradi mingine inayo fadhiliwa na shirika la misaada la Marekani ofisi ya Tanzania, NAFAKA na TUBOCHA. Shughuli za mradi huu zinatekelezwa katika maeneo ya Manyara, Dodoma, Morogoro, Iringa na Mbeya nchini Tanzania.

Wadau wa mradi huu wanatambua umuhimu wa msaada unaotolewa kupitia watu wa Marekani kupitia USAID 'Feed the Future initiative'. Pia tunawashukuru wakulima na wadau wote wa mradi kwa ushirikiano wao katika mradi pia mtandao wa uvumbuzi wa kilimo endelevu duniani CGIAR system.

Picha ya jalada: Zhuda, Shutterstock

*Kalenda hii imewezeshwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia USAID kama sehemu ya Serikali ya Marekani katika mradi wa Feed the Future. IITA na ACDI/VOCA zinawajibika kwa yaliyomo kwenye kalenda hii na wala sio msimamo au maoni ya USAID au Serikali ya Marekani.*

*Kwa taarifa zaidi: Feed the Future Tanzania - NAFAKA, Mkwawa, Ilala Street, Plot No. 274, Block No. V, S.L.P 185, Iringa, Tanzania | Simu: +255 754445480 au Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo Ukanda wa Tropiki (IITA) - Tanzania | S.L.P 34441, Dar es Salaam, Tanzania | Simu: +255 776000712 / 754643478*